

## **UONGOZI WA ENEO LA JUMLA LA KUSINI KATIKA UFANIKISHAJI WA LENGU LA UTUNZAJI NA IKOLOJIA MOJA YA TROPIKI**

Maneno Muhimu Usawa, utofauti, ujumuishwaji, wadau wa eneo, ushirikiano wa kimataifa.

### **Muhtasari**

Kuimarisha hali ya kushiriki kwa watafiti wa Eneo la Jumla la Kusini katika utunzaji na ikolojia ya tropiki ni lengo la jumuiya yetu ya kisayansi, lakini mapendekezo ya kuboresha ujumuishwaji mara nyingi yanaelekezwa katika taasisi na watafiti wa Eneo la Jumla la Kaskazini. Ingawa maboresho haya ni muhimu, kuna changamoto maalum za utofauti, usawa na ujumuishwaji (DEI, Diversity, Equity and Inclusion) ndani ya Eneo la Jumla la Kusini zinazosababishwa na miktadha yake ya kijamii na kiuchumi, utamaduni na kisayansi. Kwa hivyo, mabadiliko yanayopendekezwa kwenye Eneo la Jumla la Kusini ni muhimu kwa mabadiliko ya kudumu katika kanuni za DEI, ambayo yanahakikisha kuwa utafiti wa ikolojia ya tropiki na utunzaji unakabiliana na changamoto za sasa za utofauti. Tunapendekeza hatua kumi muhimu za kufanikisha ushirikiano wa kimataifa wenye usawa katika ikolojia ya tropiki, ambao, ukiwa unaongozwa na watafiti wa Eneo la Jumla la Kusini, unaweza kuboresha kanuni za DEI katika viwango vya kitaasisi, kitaifa na kimataifa. Katika kiwango cha kitaasisi, tunapendekeza (1) kuwa vielelezo kwa kanuni za DEI, (2) kubuni utafiti kwa pamoja na wadau wa eneo, na (3) kukuza usimamizi wa ufadhili wenye uwazi ili kupendelea wanasayansi wa eneo. Katika kiwango cha kitaifa, tunahimiza (4) kuhusishwa kwenye hatua za kisiasa za kulinda wanasayansi na utafiti wao katika nchi za tropiki, (5) kushiriki katika kuboresha sera za utafiti wa utofauti, na (6) kubuni utafiti ambao unafikia jamii. Katika kiwango cha kimataifa, tunahimiza watafiti wa Eneo la Jumla la Kusini kushiriki katika ushirikiano wa kimataifa ili (7) kuongoza na kuelekeza maombi ya ufadhili, (8) kuhakikisha wingi wa kazi unaolingana, na (9) kupigania manufaa yanayolingana kati ya washirika wa kitaifa na wa kigeni. Hatimaye, (10) tunapendekeza kwamba uongozi wa Eneo la Jumla la Kusini katika juhudi za kimataifa uwe na uwezo mkubwa zaidi wa kuboresha kanuni za DEI kimataifa, kuhakikisha mabadiliko mazuri ya kudumu katika jumuiya yetu ya kisayansi. Nyenzo za ziada zinatoa muswada huu kwa lugha nyingine zinazozungumzwa katika Eneo la Jumla la Kusini.